ANCH Professional Services Ltd

Ref: ANCH/SSNG-19/1 **16 Mei 2019**

Afisa Mtendaji,
Kijiji cha Songosongo
Wilaya ya Kilwa,

YAH: MAOMBI YA KUWA MNUNUZI WA MAZAO YA BAHARINI IKIWEMO SAMAKI, PWEZA NA AINA NYINGINE PAMOJA NA ENEO LA KUWEKA KIWANDA CHA USINDIKAJI WA MAZAO HAYO

Anch Professional Services Ltd ni Kampuni ya wazawa (wamiliki ni Gration Gervase na Rachel Henry) iliyosajiliwa Tanzania.

Kampuni hii inayo nia ya kuwa mdau wa maendeleo katika Kijiji cha Songosongo (Kilwa) kwa kufanya mambo mawili. Moja ni kuwapatia soko wavuvi walioko kijijini Songosongo kwa kununua mazao yao ya baharini hapo kijijini kwa bei ya soko (inayozingatia maslahi ya pande zote mbili) . Jambo la pili ni kuweka mitambo ya kusindika samaki/mazao ya baharini ili kuweza kusafirisha mazao/samaki hao kutafuta soko nje ya Songosongo.

Ili kufanikisha malengo hayo, Kampuni yetu inapendekeza kuwa na utaratibu/makubaliano maalum na wavuvi wa Songosongo kupitia umoja wao au Serikali ya Kijiji. Aidha, Kampuni inaomba kupewa eneo kwa ajili ya kuendesha shughuli za ununuzi na usindikaji.

Ni matumaini na matarajio yetu kuwa utekelezaji wa mambo hayo mawili utawezesha wananchi (wavuvi) kupata soko la uhakika na hivyo kuongeza/kuchochea shughuli za uvuvi. Aidha, kupanuka kwa shughuli za uvuvi na kuanza kwa usindikaji kutaongeza ajira kwa wananchi wa Songosongo.

Tunaomba ushirikiano ili tuweze kuendelea na hatua zinazofuata.

Wako katika ujenzi wa Taifa.

Gration Gervase
Mkurugenzi

10th Floor IPS Building, Samora Avenue/Azikiwe Street, P.O.Box 70166 Dar es Salaam-Tanzania
Tel: +255 673 605 481, +255 689 605 481, E-mail Address: apstz@outlook.com